Karagwe mkoani Kagera juzi. Kushoto ni Meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Baraka Ladislaus. (Na Mpigapicha Wetu).

UHURU UK 15.

# Boti ya kisasa kulinda rasilimali Ziwa Victoria

**Na BALTAZAR MASHAKA,** *Muleba*

SERIKALI mkoani Kagera imemkabidhi Ofisa Uvuvi Mwalo wa Katemve Magarini, wilayani Muleba, boti ya kisasa itakayofanya doria Ziwa Victoria, kudhibiti matukio ya uvuvi haramu na uhalifu.

Boti hiyo yenye thamani ya sh. milioni 32.9 ilikabidhiwa juzi na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge na kuwaagiza maofisa uvuviwilayani humo kuitumia kwa manufaa ya wananchi.

Aliwataka kuhakikisha inatumika kwa ulinzi wa rasilimali zilizomo Ziwa Victoria hususan eneo la visiwa vilivyopo wilayani hapa.

Meja Jenerli Mbuge aliwaeleza wananchi wa Muleba, boti hiyo imenunuliwa kupitia mapato ya kodi na kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wa nje ya nchi.

"Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kutambua umuhimu wa kutunza rasilimali na bidhaa adimu ya samaki katika ziwa letu, imeleta boti kuimarisha ulinzi ili vizazi vijavyo vikute mazalia ya samaki," alisema.

Ofisa Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Masanja Kadashi, alisema awali uvuvi haramu ulishamiri kwa kiwango kikubwa kwa sababu ya kukosekana vitendea kazi vya kudhibiti vitendo hivyo.

CamScanner



MWANANCHI UK3

# Kampuni ya bima yalenga kunufaisha wavuvi milioni 4.5

**Pamela Chilongola**, Mwananchi
pchilongola@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Kampuni ya huduma za bima ya Acclavia imeingia mkataba wa miaka mitatu na Mfuko wa Kusaidia Wavuvi Tanzania kutoa bima ya afya na maisha pindi wanapopata ajali, kupoteza vitendea kazi, kuumia au kufariki dunia wakiwa kazini.

Kwa mujibu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sekta ya uvuvi inatoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5 katika mnyororo mzima wa thamani, ambapo ajira za moja kwa moja kwa wavuvi ni 194,804 na wakuzaji viumbe maji ni 31,998.

Sekta hiyo imetawaliwa na wavuvi wadogo kwenye maji ya asili na huchangia takribani asilimia 95 ya samaki wote wanaovuliwa nchini.

Pia, sekta hiyo huchangia katika kipato cha familia pamoja na kuongeza usalama wa chakula na lishe kwa kuwa samaki huchangia asilimia 30 ya protini inayotokana na wanyama.

Akizungumza jana jijini hapa, Mkurugenzi wa Acclavia, Miradio Mpangile alisema wameingia mkataba huo baada ya kuona wavuvi wakifanya kazi huku wakiwa hawana bima inayoweza kuwasaidia pindi wanapoumwa au kupata ajali wakiwa kazini.

Mpangile alisema wavuvi watakaonufaika na bima ya matibabu na ya maisha wapo zaidi ya milioni 4.5.

"Wadau wetu tunaoshirikiana nao ni Kampuni inazotoa bima ya maisha ya Sanlam na Strategies inayoshughulika na bima ya matibabu, ambazo zitatoa huduma kwa wavuvi hao," alisema Mpangile.

Kwa upande wake Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam kutoka Mamlaka ya Bima Tanzania (Tira), Franky Fred aliwataka wavuvi hao kujiunga kwenye huduma za bima za afya na maisha kwa kuwa gharama wanazotakiwa kulipa ni kidogo.

Alisema mamlaka hiyo inaendelea kutoa mwongozo wa jinsi ya kuwafikia wananchi popote pale walipo, pindi wanapopata ajali au kuumwa ili waweze kutibiwa kwa kiasi kidogo wanacholipia.

"Mafao wanayotoa yananipa faraja, mfano leo hii mfanyakazi wa Serikali akipata tatizo la figo sekta ya bima inatoa fao hadi Sh200 milioni kwa ajili ya kutibiwa.

"Bima ni muhimu kuwa nayo kwa sababu maradhi na kifo havitoi taarifa, huja ghafla," alisema.

**SHUGHULI NYINGINE**

**Kampuni ya Acclavia vilevile hutoa huduma za bima mbalimbali, zikiwemo za magari, nyumba, biashara, usafirishaji, afya na kilimo, ikijumuisha za vikundi vya kidini, wakulima, wajasiriamali, wachimbaji madini, taasisi na asasi mbalimbali.**

**194,804**

**Idadi ya wavuvi waliopo katika ajira za moja kwa moja.**